**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MARA

**Juni, 2024**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu**
**Mkuu wa Shule 0755 47 80 30**
**Makamu Mkuu wa Shule 0768 72 86 74/0655728674**
**Mtaaluma 0752 39 32 32/0625 91 21 25**
**Shule ya Sekondari Mara,**
**S.L.P193,**
**MUSOMA.**
**Tarehe 06.05.2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………….**
**S.L.P ……………………………………..**
**……………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MARA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MUSOMA MKOA WA MARA MWAKA 2024/2025**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha tano katika Shule hii mwaka **2024/2025** na atasoma tahasusi ya ………….

Shule ya Sekondari Mara ipo umbali wa Kilometa 9 Kusini mwa mji wa Musoma. Usafiri wa pikipiki/basi kutoka stendi kuu ya manispaa ya Musoma

unapatikana katika kituo cha mabasi Bweri kwa Nauli ya Shilingi **500** kwa basi (Daladala), pikipiki ni Tsh **3,000/-** na **5,000/-** kwa bajaji.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe………… hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe… . Na…….. Mwisho wa kuripoti ni tarehe ……….

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule ni suruali nyeusi (02) kwa Wavulana. Suruali iwe na turn-up na upana wa 18cm.
ii. Mashati meupe (02) ya mikono mifupi.
iii. Sare ya Michezo ni bukta, viatu, soksi na jezi njano au nyekundu (02) kwa wavulana.
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
v. Soksi jozi mbili nyeusi za shule.
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali.
vii. Sweta rangi ya ugoro (01), (Pia zinapatikana shuleni kwa mzazi atakayenda kununua shuleni kwa Tsh 15,000)
viii. Nguo za kushindia suruali ya kijivu (02)
ix. Tisheti (T-shirt) mbili (02) rangi ya blue kola nyeusi (Pia zinapatikana shuleni kwa mzazi atakayependa kununua shuleni kila moja Tsh12,500/=).

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 6 au zaidi 3Q.
ii. Aje na nakala ya cheti cha kuzaliwa na Result slip ya kidato cha nne.
iii. **Ream (A4)** Mbili (2) kwa mwaka.
iv. Kalamu za wino za kuandikia na penseli za kuchorea HB No 2
v. Tochi ya mwanga wa sola kwa dharura pale mwanga unapokosekana.
vi. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology (Pia zinapatikana shuleni-kwa malipo)
vii. Scientific Calculator (Pia zinapatikana shuleni-kwa malipo)
viii. Godoro kwa wanafunzi wa Bweni 2 ½ x 6 x 6. (Pia yanapatikana maduka yaliyo karibu na shule).

ix. Mashuka Jozi 2 (1 pink na 1 Blue), blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 rangi ya kijani au Blue.

x. Nguo za ndani za kutosha;

xi. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);

xii. Ndoo 1 ndogo (lita Kumi) yenye mfuniko na kidumu cha maji ya kunywa cha ujazo wa lita moja.

## 2.3 Vifaa vya kazi au usafi

xiii. **WANAFUNZI WOTE** (Tahasusi zote) waje na vifaa vifuatavyo kwaajili ya usafi wa mazingira ya shule

a) Soft broom,hard broom,mopa,fagio wa chelewa, Jembe na mpini wake na dawa ya chooni (dexy all puporse cleaner lita 05)

b) Tahasusi ya PCM na HGL waje na Aro (Dawa) na mifagio migumu ya kusugulia uchafu kwenye matundu ya vyoo

c) Tahasusi ya HGE, EGM, na PGM waje na Panga moja.

d) Tahasusi ya HKL na CBG waje na Koleo moja (yenye mshikio wa chuma)

e) Tahasusi ya PCB waje na sururu moja (yenye mpini wake)

f) Tahasusi ya HGK waje na shoka moja (yenye mpini wake)

**<u>NB</u>**: Matibabu; Mwanafunzi aje na Bima ya Afya ya NHIF, AAR au 50,400 kwa ajili ya kujiunga na bima ya afya ya NHIF (**NI LAZIMA**)

## 2.4 Michango mbalimbali

### a) Shule za Bweni

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi | AKAUNTI YA MALIPO |
|---|---|---|---|
| 1 | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000 | NMB - 30301100042<br>JINA: **MARA SECONDARY** |
| 3 | Tahadhari | 5,000 | |
| 5 | Nembo | 5,000 | |
| 6 | Kitambulisho cha Shule | 5,000 | |
| | **Jumla** | **80,000** | |

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na SIMU SHULENI kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kumpiga , kupigana na mwanafunzi mwenzake, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi.
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe
ix. Uvutaji wa sigara; (matumizi ya dawa za kulevya)
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia **SIMU YA MKONONI** (Ndani na Nje ya mazingira ya shule)
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; nk
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

4. **Viambatisho na Fomu Muhimu**
   i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
   ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
   iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
   iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI MARA**

**Saini ya Mkuu wa Shule ……………………………………….**

**Jina la Mkuu wa Shule GINOGA MUSTAFA MAKONGORO**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ..** HEADMASTER MARA SEC. SCHOOL MUSOMA **..**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKA[illegible]ONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0755 47 80 30**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0768 72 86 74/0655728674**
- **Mwandamizi Taaluma 0752 39 32 32/0625 91 21 25**
- **Mwandamizi Malezi 0683 48 42 52**

# FOMU YA HISTORIA YA MWANAFUNZI

1. JINA ………………………………………………….......... DINI ………………………………………..........
2. TAREHE YA KUZALIWA………………………........…3. KIJIJI ULIMOZALIWA……………………........
4. TARAFA ULIMOZALIWA ………………… .......5. WILAYA ULIMOZALIWA ………….........
6. MKOA ULIMOZALIWA ……………………........ KAMA UNAKAA MJINI …………….........
7. TAJA MJI:………………………..........MTAA………………..BARABARA……………….........
8. JINA LA BABA……………………………….9. KAZI YA BABA……………………....................
10. ANWANI YA BABA……………………………………………………………………………........................
11. JINA LA MAMA ……………………………........ 12. KAZI YA MAMA………………………...........
13. ANWANI YA MAMA ………………………………………………………………………......................
14. JINA LA ATAKAYEHUSIKA NA MWANAFUNZI KIPINDI CHOTE CHA MASOMO:

    JINA:.................................................................... ANWANI:............................................................................

    SIMU:............................................................ EMAIL: ...........................................................................

15. SHULE ULIZOSOMA | MADARASA | MADARAKA ULIYOSHIKA

| SHULE ULIZOSOMA | MADARASA | MADARAKA ULIYOSHIKA |
|---|---|---|
| …………………………… | ………………… | ………………………………… |
| …………………………….. | ………………… | ………………………………… |

16. JE, BABA YU HAI? ……………………….............. (NDIYO/HAPANA)
17. JE, MAMA YU HAI? ……………………….............. (NDIYO/HAPANA)
18. JE, UNAKAA NA MLEZI …………………................ (NDIYO/HAPANA)
19. ANWANI YA MLEZI ……………………………………………………………………
20. KAZI YA MLEZI …………………………………………………………………………
21. ELEZA MATATIZO YA NYUMBANI, YA MAGONJWA, N.K. YANAYOKUKABILI

    ……………………………………………………………………………………………………...........

22. UNAFIKIRI MATATIZO HAYO YATATATULIWA VIPI? ………………………….................

    ………………………………………………………………………………………………..............

23. ELEZA MIPANGO YAKO YA MAISHA YA BAADAYE

    ………………………………………………………………………………………………..............

24. MKO WANGAPI KATIKA FAMILIA? (A) WA KIUME …………………………………...............

    (B) WA KIKE ……………………….. (C) WEWE NI WA NGAPI ………………….................

    (D) NDUGU WANGAPI WAMEAJIRIWA ? ………………………………………………..............

25. KAZI AMBAZO UNGEPENDA KUFANYA BAADA YA KUMALIZA MASOMO

    ………………………………………………………………………………………………..............

26 KAZI AMBAZO USINGEPENDA KUFANYA BAADA YA KUMALIZA MASOMO

    ………………………………………………………………………………………………..............

26. JINA …………………………………… SAHIHI……………… TAREHE……………................

# MEDICAL EXAMINATION FORM

To be Completed by a Medical officer in respect of all one(s) new entrants

Full Name: ......................................................................................................

Age............................................. Year ....................................Sex.......................

Blood count (Red and white)..........................................................................

Stool examination.........................................................................................

Urine analysis...............................................................................................

Syphilis Test.................................................................................................

T.B Test........................................................................................................

Ears...............................................................................................................

Chest.............................................................................................................

Spleen...........................................................................................................

ADDITIONAL INFORMATION e.g Physical detects or impairment Infections, Chronic of family diseases etc.

......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

From the results shown above. I certify that the above student is fit/unfit to pursue studies.

Signature.......................................................................................

Designation...................................................................................

Station...........................................................................................

## AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi..........................................................................................................................................

Nimesoma na kuelewa yote yaliyoelekezwa kwenye barua ya kujiunga na shule.

Ninaahidi kuwa nitajifunza kwa bidii zangu zote, nitazingatia sheria za shule kama zilivyoainishwa, nitazifuata na nitakuwa na nidhamu wakati wote kwa manufaa yangu, ya shule na ya taifa kwa jumla.

| | | |
|---|---|---|
| ................................................. | .............................. | ............................................... |
| **Saini ya Mzazi/Mlezi** | **Tarehe** | **Saini ya Mwanafunzi** |

**VITABUMUHIMUKUWANAYO**

**PHYSICS**

1. Advanced level Physics 6th edition by Nelkon and Parker (1989)- Muhimu
2. Advanced Physics by Tom Duncan
3. Advanced level Physics paper 1 and paper2 by E. Njau (2002)
4. Principle of physics for class XII & XI by S.Chand (2011)
5. A-level Physics four the edition by Roger Muncaster (fourthedition)(1993)

**NB.** Angalau ununue kimoja

**MATHEMATICS**

1. **Scientificcalculators**
2. Basic and Applied mathematics by Respicius Kiiza(2010)
3. Mathematics for class Xi & XII by DASS,H.K & VERMA,R.(2000)
4. Pure mathematics (revisededition) by M.F Macrae ( 2011)
5. Pure Mathematics Volume 1 & 2 by Backhouse,J.K (1985)
6. Core Mathematics for Advanced level by L.Bostock
7. Advanced level Mathematics by L.K.Shayo
8. Advanced level Mathematics Vol.1 & II by Kinunda (1974)

**NB:** Angalau ununue kimoja

**BIOLOGY**

1. Dissecting kit- Muhimu
2. New understanding Biology for A-level student by Glenn&s.Toole (1999)
3. Systematic and classification by L.K.Msaki (1993)
4. Biology, A functional Approach by M.B. V Roberts ( 1971)
5. Advanced Biology: Principle and Application by C.J. Clegg & D. G. Mackean (2000)
6. Biological Science by Taylor,etal (1997)- Muhimu
7. S.Chand's Biology for class XI & XII byP.SVerma & B.P Pandey (2005).
8. Guide to dissection by H.G.Q Rowett (2005)

**CHEMISTRY**

1. Advanced Chemistry Physical and industrial by P.Mathew(2006)
2. Essentials of physical chemistry by Arun Bahil,B.S Bahil & G.D Tuli(2012).
3. Organic Part **A & B** by A.Abdullah & M.H.Nkunya.
4. Inorganic **Part A & B** by J.S Maro Guterman & M. Mikesewala (1989)
5. Physical Chemistry by D dungu & J.B.A Mihigo (1998)
6. Advanced level Inorganic Chemistry **PART I &II** by Tanzania Institute of Education ( 1995 )
7. Organic Chemistry an introduction by Jack E.Fernandez ( 1982)
8. Understanding Chemistry for A-level student
9. Conceptual chemistry for class XII & XI by S.K Jaini(2011).
10. Advanced level chemistry,four the dition by E.N Ramsdens(2000)